

Ujinsia Katika Kiswahili Cha Vijana

Anandumi S. Mbise
Usa-River, Arusha-Tanzania
John Musyoka Mutua
Department of Linguistics and Languages
Machakos University, Kenya.

IKISIRI

Dhima kuu ya lugha ni mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Aidha, kuna mambo kadhaa yanayoamua jinsia lugha inavyotumika katika jamii kutegemea lengo, miktadha, tabaka, jinsia na umri wa wahusika katika mawasiliano miongoni mwa viamuzi vingine. Wataalamu mbalimbali kama vile: King'ei na Kobia (2007), King'ei (2010), Matinde (2012) na Mohammed (2013) wameonesha kwamba lugha ya Kiswahili inadhihirisha jinsia kuwa ni ya kiume au ya kike kwa kutumia kigezo kimoja tu cha kutaja majina mahususi ya wahusika kama vile; Juma (kiume) na Asha (kike) na siyo vinginevyo. Hivyo, huwezi kutambua jinsia ya mtu bila kutaja jina mahususi la mhusika (JMLM). Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza jinsi Kiswahili cha vijana kinavyoweza kubainisha jinsia bila kutaja JMLM. Ni kwa mantiki hii, ambapo lengo la makala hii ni kubainisha misamiati inayodhihirisha jinsia katika Kiswahili cha vijana na pia kufafanua sababu za utumizi wa misamiati hiyo. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Utambulisho wa Kijamii iliyoasisiwa na Turner mwaka (1979) na kuungwa mkono na Tajfel (1980) ambapo msingi wake ni kueleza namna kundi la watu katika jamii linavyounda umoja wao na kujipambanua na kujitofautisha na makundi mengine ndani ya jamii kwa kuzingatia namna wanavyotumia lugha. Utafiti ulifanyika katika wilaya ya Meru, kata za Kikatiti, Maji ya Chai na Usa-River; mkoa wa Arusha-Tanzania. Data zilikusanywa uwandani kwa mbinu ya Hojaji na Mahojiano. Mbinu hizi zilitumiwa kwa watoa taarifa ambao ni vijana wa umri miaka 18-35 wa jinsia zote (kike na kiume) wa viwango vyote vya elimu bila kujali hali zao za kiuchumi wala tabaka. Utafiti ulionesha kuwa asilimia kubwa ya vijana wana uelewa wa msamiati unaodokeza jinsia bila ya kutumia jina halisi la mhusika. Kwa hivyo, utafiti umeonesha tofauti baina ya uzungumzaji wa vijana na makundi mengine ya jamii moja na pia sifa ya uana.

VIVUFISHO

JHLM: Jina halisi la mhusika

KKS: Kamusi ya Kiswahili Sanifu

KCV: Kiswahili cha Vijana

BAKIZA: Baraza la Kiswahili Zanzibar

Date of Submission: 18-06-2020

Date of Acceptance: 06-07-2020

I. UTANGULIZI

Jinsia ni kategoria ya sarufi mapokeo ambayo hubainisha maumbile katika tungo. Kwa mujibu wa isimujamii zipo aina mbili za jinsia, ambazo ni: - jinsia ya kibaiolojia na jinsia ya kisarufi. Jinsia ya kibaiolojia ni ile inayohusu maumbile ya mtu kuwa ya kike au wa kiume na kikawaida aina hizi husawiriwa na lugha. Kwa mfano lugha ya Kiingereza ina maneno kama vile: *Patron, He, Boy, na Headmaster* ambayo hudokeza jinsia ya kiume ilihali maneno kama vile: *matron, she, girl na headmistress* hudokeza jinsia ya kike Matinde (2012).

Endapo mtu akizaliwa na jinsia ya kike huitwa mke na akizaliwa na jinsia ya kiume huitwa mume kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004). Hata hivyo tunatambua kuwepo kwa jinsia ya tatu iliyo na watu wachache (hundha) waliozaliwa na kasoro za kibaiolojia na ambao hawakuzingatiwa katika utafiti huu.

Dhana ya kijana imekuwa ikifasiliwa kulingana na vigezo mbalimbali vikiwemo vigezo vya kidini, kiutamaduni, umri, kisaikolojia pamoja na kigezo cha kiserikali. Kwa kutumia kigezo cha umri dhana ya kijana imefafanuliwa na BAKIZA (2010: 165) kuwa "*Kijana ni mtu mwenye umri wa baina ya utoto na makamo*".

Wataalamu mbalimbali wameeleza dhana ya jinsia na utumizi wa lugha ya Kiswahili kwa namna ambavyo inaonekana kuwa lugha ya Kiswahili haiwezi kudhihirisha jinsia (kiume au kike) katika utumizi wake bila kutumia JHLM ambalo ndilo linalobainisha kuwa mhusika fulani ni wa kike au wa kiume. Lakini swali ambalo watafiti wanapania kulishughulikia ni je, ni kweli kuwa Kiswahili hakiwezi kudokeza jinsia bila ya kutumia JHLM kama ilivyo kwa lugha za Kifaransa, Kiingereza na lugha zingine?

Kwa mujibu wa King'ei (2010:17) katika kitabu chake cha *Misingi ya Isimujamii*, alikuwa akizungumzia tofauti katika matumizi ya lugha ya wanaume na wanawake, alibaini mambo ambayo yanaathiri lugha kuwa ni pamoja na: - cheo, kiwango cha elimu, mazingira, hali ya mhusika, njia ya mazungumzo na uana. Alieleza kuwa kuna tofauti ya uzungumzaji kati ya wanaume na wanawake na bila ya mifano alieleza kuwa lugha ya wanawake hudhihirisha unyenyekevu, upole na uadilifu. Kinyume na wanaume ambao lugha yao hudhihirisha kiburi, maamrishi na kujiamini. Maelezo haya ya King'ei (2010) yanabeba sifa za jumla zinazojitokeza katika tofauti ya uzungumzaji kati ya wanawake na wanaume, na kwa kuwa dunia ni pana na yenye utamaduni tofauti tofauti basi na lugha sharti itofautiane miongoni mwa jamii moja na nyingine au kundi moja na lingine katika jamiilugha moja.

Lugha ni nyenzo kuu ya mawasiliano katika jamii na hutumiwa kwa namna tofauti katika miktadha mbalimbali. Hivyo, kuelewa lugha ya jamii kunaendana na kuelewa jamii yenyewe ikiwa ni pamoja na kuyaelewa matabaka na makundi anuai yaliyomo ndani ya jamii kama vile vijana, wazee, wanawake, wanaume, wanafunzi, wanamichezo, wanajeshi, waalimu na wengine. Kwa mujibu wa Bright (1965) kila kundi la watu katika jamii hutumia lugha inayolitambulisha tabaka au kundi hilo.

II. LUGHA NA JINSIA

King'ei (2010) na wengine walieleza kuwa Kiswahili hakiwezi kudokeza jinsia kwa namna yeyote ile pasipo kutumia jina halisi la mhusika. Alifafanua kuwa uhusiano baina ya lugha na jinsia ni suala muhimu sana. Binadamu hufunzwa na jamii kwa kutumia lugha ili waweze kujifahamu wao ni kina nani. Kwa hiyo kuna ukuruba mkubwa kati ya lugha na jinsia. Anaeleza kuwa kwa mfano lugha ya Kifaransa ina nomino maalumu za kurejelea wanawake na wanaume. Pia Kiingereza kinazo nomino kama hizo ambazo huonesha iwapo mhusika ni mwanaume au mwanamke. Kwa mfano maneno kama vile: *she, he, his, her, hers*, na *him* huashiria mgao huu wa jinsia katika lugha ya Kiingereza jambo ambalo wataalamu walisema kuwa halipo katika lugha ya Kiswahili. Tafiti nyingi zilizohusu lugha ya Kiswahili kwa mfano, Matinde (2012) katika *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia* alieleza kuwa hali kama hiyo haipo katika Kiswahili. Jambo ambalo liliwasukuma watafiti kuchunguza lugha ya vijana ikiwa madai hayo ni ya kweli.

Coates (1986) alifanya utafiti ujulikanao kama "*Women, Men, and language: A social linguistics account of gender differences in language*" akichunguza namna lugha ya wanaume na wanawake na jinsia zianavyoathiriana, alianza kwa kueleza kuwa lugha haina jinsia lakini lugha inaweza kutumiwa kuonyesha uana katika jamii. Alizidi kueleza kuwa jinsia ni neno linalotumiwa kuelezea mambo yote yanayohusiana na hali ya kuwa mke au mume. Alidai kuwa sifa inayobainika kati ya lugha na jinsia ni mielekeo ya watu tu kuhusu maneno fulani katika lugha husika. Hata hivyo utafiti wake huu unadokeza jambo moja la muhimu ambalo ni tofauti na wataalamu wengine kuwa lugha haina jinsia bali lugha yaweza tu kutumiwa kudokeza jinsia, hili ni jambo lenye kuleta wazo lenye kuvutia kuchunguzwa. Utafiti wake ulichangia pakubwa katika kuchunguza namna jinsia inavyodokezwa kwenye lugha fulani kwenye lugha ya Kiswahili.

Naye Jespersen (1949) katika utafiti wake aliouita "*Americans structural linguistics*" (mitindo ya lugha za Wamarekani) alichunguza mitindo ya lugha kwa kulinganisha mazungumzo ya wanawake na wanawake me wa Kimarekani. Uchunguzi wake ulionyesha kuwa, wanawake wanaingilia mazungumzo sana wakati wa kuzungumza jambo ambalo linasababisha kutumia sentensi ndefu zisizo na ukomo. Kwa mujibu wa utafiti wake alieleza kuwa hali hiyo huwa inatoa nafasi kwa mtu mwingine kuingilia mazungumzo na kuendelea na jambo linalozungumzwa. Kwa kufanya hivyo, utafiti wake ulieleza kuwa wanawake huwa wanavunja sheria ya mazungumzo ambayo humtaka mzungumzaji wa kwanza kumaliza ndipo mzungumzaji mwingine afuate. Kwa mujibu wa utafiti wake alieleza kuwa jambo hili ni tofauti kabisa na wanaume ambao wao huwa wanapeana nafasi ya kuzungumza na kumaliza. Mchango wake ni muhimu kwa kuwa tofauti ya kuzungumza baina ya wanawake na wanaume itasaidia kubaini ni jinsia gani huwa na tabia ya kuzungumza zaidi na hivyo kuwa na uwezo mkubwa wa kupata msamiati mwingi kiasi hata cha kuwa na msamiati ambao unaweza kutumika kudokeza jinsia fulani bila kutaja JHLM.

Kadhalka, Haas (1978) alichunguza tofauti ya mazungumzo ya wanawake na wanaume kama inavyoonekana katika jamii. Utafiti wake ulihusisha tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu matumizi ya lugha ya wanawake na wanaume. Matokeo ya utafiti wake yameonesha kuwa mazungumzo ya wanawake na wanaume yanatofautiana katika mitindo, mada, maudhui, na matumizi. Pia ameeleza kuwa mazungumzo ya wanawake yanatumia lugha ya upole, pia wanatumia maneno yenye kueleza hisia, maneno yenye kuomba radhi, sentensi zisizomalizika na mazungumzo yao yanahusu habari za nyumbani na familia. Lakini kwa upande wa wanaume alieleza kuwa wao wanatumia lugha isiyo sanifu, si wasemaji sana na mazungumzo yao yanahusu michezo, pesa, na biashara, na wanatumia maneno ya mkato. Hivyo kwa mujibu wa utafiti wa Haas (keshatajwa) umeeleza tofauti ya lugha ya wanawake na wanaume kwa ujumla, bila ya kuonesha tofauti hizo katika jamii mahususi kama jamii ya wanaozungumza Kiswahili.

Juma (2015) alichunguza tofauti ya kijinsia katika utumiaji wa lugha ya Kiswahili kwa vijana wa kike na wa kiume Zanzibar. Katika utafiti wake amebainisha kuwa vijana wa kiume wanatumia lugha ya ulaghai

wanapokuwa na vijana wa kike kwa lengo la kukubaliwa matakwa yao. Pia alibainisha kuwa wanaume wanafupisha maneno katika mazungumzo yao. Mfano neno *shem* badala ya *shemeji* (uk.12). Pia ameeleza kuwa wanaume katika mazungumzo yao wanachanganya lugha ya Kiswahili na Kingereza. Kwa mfano, *naona unainjoy* (uk.11). Utafiti wa Juma umeegemea zaidi katika kuangalia matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa vijana wa kike na wa kiume, na umeleza jinsi vijana hao wanavyoitumia lugha hiyo katika jamii. Uchunguzi wake haukueleza sababu za kuwepo na tofauti wa uzungumzaji miongoni mwa makundi katika jamii.

Broadbridge (2003) alichunguza tofauti ya mazungumzo baina ya wanawake na wanaume wanaofanya kazi shule moja kwa kipindi kirefu huko Tokyo Japan. Matokeo ya utafiti wake yalionesha bila kutumia mifano kuwa, wanaume wana tabia ya kuingilia kati mazungumzo ya wanawake, pia wanaume wanatumia zaidi maneno ya viapo kuliko wanawake na pia wanaume wanatumia zaidi maneno ya kutupa tupa zaidi ya wanawake. Kwa upande wa wanawake na utumizi wa lugha alibainisha kuwa wanawake wanatumia zaidi viashiria vya msikilizaji kama vile: - mmh, ndio, sawa na kadhalika. Aidha, Labov (1966) alitafiti kuhusu Mgawanyiko wa Kingereza katika jamii ya New York, Marekani. Aligundua kuwa wanaume wanatumia sana maneno ya misimu yaani maneno yanayozuka na kutoweka katika jamii, ambayo huzushwa na kikundi cha watu wachache. Alieleza sababu ya kutumia lugha hiyo isiyo rasmi miongoni mwa wanaume kuwa ni kuficha jambo fulani ambalo halitakiwi kufahamika na watu wote. Kinyume na wanawake ambao katika matumizi yao ya lugha hawatumii sana misimu badala yake hutumia lugha fasaha. Utafiti huu ulichangia kuonesha mojawapo ya sababu ya kutumia lugha isiyo sanifu miongoni mwa wanaume kuwa ni ili kuficha ujumbe kwa wasiokusudiwa ikiwa hii ni mojawapo wa sababu za utumizi wa lugha kijinsia.

Msanjila, Kihore na Massamba (2009) walieleza sababu za kundi fulani katika jamii hutumia mtindo tofauti wa uzungumzaji katika jamii kwa lengo la kujitambulisha. Wanaeleza kuwa, kundi la watu, jamii au taifa fulani hujibainisha kuwa ni tofauti na kundi, jamii au taifa lingine kwa kutumia mtindo tofauti ambao huweza kuwapambanua wao na kuwatofautisha na wengine.

III. NADHARIA YA UTAMBULISHO WA KIJAMII

Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii iliasiswiwa na Turner (1979) na kuungwa mkono na Tajfel miaka ya 1980. Kwa mujibu wa Nadharia hii ya Utambulisho wa Kijamii inaeleza jinsi kundi la watu katika jamii linavyounda umoja wao na kujipambanua na kujitofautisha na kundi lingine ndani ya jamii moja kutokana na matendo wanayoyafanya au kutokana na mtindo wa kuzungumza wanaoutumia. Makundi haya ya kijamii huweza kuzuka kutokana na tofauti za kielimu, kiumri, kiuchumi, kazi wanayofanya na mahusiano ya wazungumzaji wa lugha hiyo. Hivyo utafiti huu ulilenga kupata taarifa toka kwa vijana wenye umri wa kuanzia miaka 18-35 wa jinsia zote (kike na kiume) wa viwango mbalimbali vya kielimu bila kujali hali zao za kiuchumi na kitabaka. Hivyo, kwa kutumia nadharia hii ni dhahiri kwamba utafiti huu uliweza kubaini ni jinsi gani kundi la vijana katika jamii linavyounda umoja wao na kuweza kujipambanua na kujitofautisha na makundi mengine ndani ya jamii moja kiasi kwamba kwa kutumia mtindo wao wa uzungumzaji lugha, wameweza kudokeza jinsia fulani bila ya kutumia JHLM.

Halikadhalika, utafiti huu umeongozwa na mhimili uitwao ujumuishi, ambao unaeleza kuwa kuchunguza uhusiano wa lugha na jamii hakujikiti kumuangalia mtu mmoja mmoja katika jamii, bali kuangalia watu wanaounda kundi fulani kwa pamoja. Hii ni sifa ya muhimu kwa utafiti huu kwani nadharia hii ilisaidia kujua hisia, tabia na matamano ya kundi la vijana wenye umri wa miaka 18-35 katika jamii. Kutokana na ufafanuzi huu ndio maana mkazo uliwekwa kuona ni kwa namna gani lugha ya kundi hili la vijana ilivyodokeza jinsia katika utumizi wake.

IV. MSAMIATI UNAODOKEZA JINSIA KATIKA KISWAHILI CHA VIJANA

Ili kubainisha misamiati inayodokeza jinsia katika Kiswahili cha vijana tulitumia mbinu ya hojaji ambapo maswali yaliandaliwa katika jedwali na kukabidhiwa watoa taarifa. Maelekezo kwa watoa taarifa yalikuwa hivi: ***Weka alama ya vyema kama msamiati ulioorodheshwa unadokezwa na jinsia iliyotajwa kwenye mabano ama weka alama ya kosa kama msamiati huo haudokezi jinsia husika.*** Watoa taarifa walijibu kama inavyodhihirika katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na.1. Majibu ya watoa taarifa kuhusu jinsia inayodokezwa na msamiati ulioorodheshwa

Msamiati	Jinsia inayodokezwa	Idadi na asilimia ya waliokubali		Idadi na asilimia ya waliokataa		Idadi na asilimia ya wasiojua	
Msela	Kiume	55	92%	36	6%	12	2%
Chalii	Kiume	57	96%	6	1%	2	3%
Demu	Kike	59	98%	6	1%	1	1%
Shoga	Kike	48	80%	10	16%	2	4%
Shosti	Kike	59	99%	0	0%	1	0%

Arifu	Kiume	48	80%	12	2%	11	18%
Manzi	Kike	59	99%	1	1%	1	1%
Shosti	Kike	60	100%	0	0%	0	0%
Mpenzi	Kike	30	50%	30	50%	0	0%
Njemba	Kiume	60	100%	0	0%	0	0%


Chanzo: Data za uwandani (Juni 2019).

Kama Jedwali Na.1.hapo juu linavyoonesha kuwa idadi na asilimia ya watoa taarifa waliokuwa na uelewa wa jinsia zinazodokezwa na msamiati uliotajwa na watafiti ilikuwa ni kubwa. Kwa kila msamiati uliotajwa watoa taarifa waliweka alama ya vyema au kosa kama utafiti ulivyohitaji. Kwa mfano, idadi ya waliosema kuwa msamiati *msela* unadokeza jinsia ya kiume walikuwa jumla ya watoa taarifa 55 ambao ni sawa na asilimia 92% ya watoa taarifa wote, waliosema msamiati huo unadokeza jinsia ya kike ni watoa taarifa 36 ambao ni sawa na 6% wakati wasiofahamu msamiati huo unadokeza jinsia gani walikuwa jumla ya watoa taarifa 12 ambao ni sawa na asilimia 2%. Kwa upande wa msamiati *shosti* kwa mfano, idadi ya waliosema ni jinsia ya kike inayodokezwa ilikuwa watoa taarifa 59 ambao ni sawa na asilimia 99% ya watoa taarifa wote, waliosema *shosti* inadokeza jinsia ya kiume ilikuwa mtoa taarifa 0 ambao ni sawa 0% wakati waliosema hawajui jinsia inayodokezwa na msamiati huo alikuwa mtoa taarifa 1 ambaye ni sawa na asilimia 0% Hivyo utafiti ulifanya hesabu inayofanana na hii kwa kila msamiati katika misamiati yote iliyokuwa imeorodheshwa. Kwa upande wa msamiati *shoga* na *mpenzi* ilionekana kuwa na utata miongoni mwa watoa taarifa kwa sababu ya misamiati hiyo kuonekana kudokeza jinsia zote. Sababu ya kuwepo kwa tofuti za uelewa wa jinsia zinazodokezwa na msamiati huu uliokuwa umeorodheshwa ni kutokana na uelewa tofauti miongoni mwa vijana, pia suala la mtoa taarifa mmoja kuwa na uwezo wa kujichanganya na wenzake kwa ukaribu zaidi kulipelekea wale wasiojichanganya kutokuelewa sana msamiati unadokeza jinsia katika KCV ili hali wale walioweza kujichanganya wakiwa na uwezo mkubwa wa kuelewa msamiati na jinsia inayodokezwa na msamiati huo kwa urahisi.

Aidha utafiti ulitumia mbinu ya mahojiano kutaka kufahamu msamiati mwingine unaoweza kudokeza jinsia kutoka kwa vijana. Swali lililoulizwa lilikuwa linasema: ***Nitajie misamiati mitano zaidi ya ile iliyotajwa na hojaji unaotumiwa na vijana kudokeza jinsia katika utumizi wao wa lugha.***

Majibu ya swali hilo yaliibuka na msamiati mwingine nje ya ule uliokuwa umeorodheshwa na utafiti Kielelezo Na. 1 kinafafanua majibu ya watoa taarifa hao

Kielelezo Na. 1.Msamiati mwingine unadokeza jinsia nje ya ule uliotajwa na utafiti



Chanzo: Data za uwandani (Juni 2019).

Msamiati kama vile: *mshikaji*, *mpenzi*, *jamaa*, *njemba*, *jembe*, *swaiba*, *mchizi* na *mwaya* ni baadhi ya msamiati mwingine ulioonekana kudokeza jinsi katika Kiswahili cha vijana ambao ndio waliokuwa watoa taarifa. Katika kielelezo Na.1 hapo juu asilimia hizo zilipatikana kwa kuchukua idadi ya watoa taarifa waliotaja msamiati husika kisha idadi yao ikagawanywa kwa sitini (60) ambayo ni jumla ya watoa taarifa na kisha kuzidishwa kwa mia moja. Hivyo ni wazi kuwa jumla ya watoa taarifa 12 ambao ni sawa na 20% waliweza

kutaja msamiati *swaiba* wakati wa mahojiano na kusema ni msamiati unadokeza jinsia ya kiume, watoa taarifa wapatao 12 ambao ni sawa na 20% walitaja msamiati *jembe* kuwa ni msamiati unadokeza jinsia ya kiume, watoa taarifa wapatao 10 ambao ni sawa na 17% walitaja msamiati *njemba* kuwa ni msamiati unadokeza jinsia ya kiume katika Kiswahili cha vijana, na jumla ya watoa taarifa wapatao 13 ambao ni sawa na 22% walitaja msamiati *mwaya* kuwa unadokeza jinsia ya kike na kundi la mwisho ni lile lenye watoa taarifa wapatao 13 ambao ni sawa na 21% waliotaja *mchizi* kuwa ni msamiati unadokeza jinsia ya kiume. Sambamba na hayo, mtafiti alipofanya mahojiano ya ana kwa ana na watoa taarifa wa kiume kutoka kila kata iliyoteuliwa, watoa taarifa waliohojiwa walieleza yafuatayo kuhusiana na msamiati mwingine unaotumiwa na vijana kudokeza jinsia:

Mtafiti: Je, ni msamiati gani nje ya huu uliorodheshwa ambao unaweza kutumiwa kudokeza jinsia katika Kiswahili cha vijana?

Mtoa taarifa X (Kikatiti) "... maneno kama vile *jembe* na *njemba* ni baadhi ya maneno ambayo tunatumia tukiwa tunamaanisha mwanaume mwenzetu na sio msichana..."

Mtoa taarifa Y (Maji ya Chai) "... *mshikaji* ni neno linalomaanisha mwanaume, pia *swaiba* linakuwa na maana ya mwanaume linapotumika kwa vijana kama sisi..."

Mtoa taarifa P (Usa-River) "...*Jamaa* na *mchizi* ni maneno yanayomaanisha mtu wa jinsia ya kiume yanapotumika..."

Chanzo: Data za uwandani, Julai 2019

Vilevile utafiti ulifanya mahojiano na jinsia ya kike kutoka katika kila kata kufahamu ni msamiati gani wanaotumia kudokeza jinsia nje na msamiati uliokuwa umetajwa na utafiti na majibu yao yalikuwa ni kama ifuatavyo:

Mtoa taarifa A (Kikatiti) "... *Mwaya* ni msamiati tunaotumia kumuelezea mtu wa jinsia ya kike

Mtoa taarifa B (Maji ya Chai) "...*Shoga* ni msamiati unaotumiwa na wasichana kumaanisha jinsia ya kike..."

Mtoa taarifa C (Usa-River) "...*Mpenzi* ni msamiati wanaotumia wasichana na wanawake kujibainisha wao kwa wao na siyo jinsia ya kiume..."


Chanzo: Data za uwandani (Julai, 2019)

6. Sababu za Utumizi wa lugha inayodokeza Jinsia miongoni mwa Vijana

Ili kubaini sababu za utumizi wa msamiati unadokeza jinsia katika Kiswahili cha vijana, mbinu ya hojaji ilitumika. Tuliwauliza watoa taarifa swali hili; **Ni sababu gani zinazofanya vijana kutumia Kiswahili kinachodokeza hali ya mtu ikiwa ni msichana au mvulana?**

Kielelezo Na.1.1 kama inavyoonekana hapo chini kinafafanua data za watoa taarifa toka uwandani

Kielelezo Na.1.1 Sababu za Vijana kutumia Lugha inayodokeza Ujinsia.



Chanzo: Data za uwandani (Juni 2019).

Kielelezo namba 1.1 hapo juu kinavyobainisha, ni wazi kuwa kuna sababu kadha wa kadha ambazo zimeonekana kuwa ndizo kichocheo cha vijana kutumia lugha ya Kiswahili kinachodokeza jinsia. Sababu iliyoonekana kuwa na mashiko zaidi kwa mujibu wa taarifa za uwandani ni kuwa: Kuficha jambo kwa

wasiohusika ndio sababu kubwa zaidi ambapo jumla ya watoa taarifa 34 ambao ni sawa 57% ya watoa taarifa waliweza kuiandika. Hii ikiwa na maana kwamba kama mtu si kijana na hausiki na kile kinachosemwa na vijana ndipo vijana huamua kuficha jambo kwa mtu huyo ili asiweze kuelewa kinachozungumzwa.

Kwa mfano vijana kutumia sentensi hii “*manzi akija mpe*” (chanzo: mtoa taarifa kutoka kata ya Kikatiti) kwa kundi ambalo sio la vijana hawawezi kujua ni nani huyo ambaye ameambiwa akija apewe, bali kwa kundi la vijana wataweza kung’amua kuwa ni msichana ndiye aliyekuwa anarejelewa na msamiati *manzi* kama ulivyotumika. Sambamba na hilo, sababu na haja ya vijana kujipambanua na kujitambulisha kuwa wao ni kundi tofauti na makundi mengine ya kijamii ni sababu iliyowafanya vijana kutumia lugha hii inayodokeza jinsia. Pamoja na hayo, sababu nyingine ni kukuza lugha ambayo ilitajwa na jumla ya watoa taarifa wapatao 9 ambao ni sawa na 15% wakitoa sababu ya kuwa na ubunifu katika kuzungumza na hiyo kuonekana kama njia kukuza na kutumia msamiati unaodokeza jinsia. Kundi lingine la watoa taarifa ni lile ambalo lilidai kuwa vijana hawana sababu yeyote ya kutumia lugha hii inayodokeza jinsia katika utumizi wake, ambapo jumla ya watoa taarifa 2 ambao ni sawa na 4% walitetea hoja hiyo.

V. HITIMISHO

Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba, Kiswahili cha vijana kinaweza kubainisha mhusika kuwa ni wa jinsia ama ya kike au ya kiume bila ya kutumia jina halisi la mhusika. Maneno yafuatayo yanatumiwa na vijana kurejelea jinsia ya kiume: Mchizi, Mshikaji, Arifu, Njemba, Swaiba, Jamaa, Chalii na Msela. Halikadhalika, kwa kutajia jinsia ya kike vijana wanatumia misamiati ifuatayo: Manzi, Demu, Shoga, Mpenzi, Shosti, Mtoto na Mwaya.

Pia kwa upande wa sababu za utumizi wa lugha inayodokeza jinsia miongoni mwa vijana ni wazi kuwa vijana waliweza kuandika sababu kadha wa kadha katika hojaji ambazo ndizo zinazosababisha vijana kutumia Kiswahili kinachodokeza jinsia. Sababu hizo zilikuwa ni pamoja na kuficha jambo kwa wasiohusika (watu wasio vijana), vijana kutaka kujipambanua na kujitofautisha na makundi mengine yaliyoko katika jamii (ambayo si vijana) na ambayo mathalani hutumia lugha ya kawaida katika kuwasiliana. Vivyo hivyo, lengo la kukuza lugha lilionekana kuwa mojawapo wasababu muhimukwa vijana ili kuwawezeshawawe na lugha yao iliyo tofauti na ile inayotumiwa na makundi mengine katika jamii.

Imebainika pia kuwa lugha haina jinsia bali ni matumizi yake miongoni mwa jamii ambayo yanaweza kudhihirisha jinsia ya mzungumzaji. Uhusiano uliopo kati ya lugha na jinsia ni mielekeo ya watu kuhusu maneno fulani katika lugha husika, yaani neno linapotumiwa linaweza kuashiria mtu wa jinsia mahsus. Aidha, kundi fulani la watu, jamii au taifa huamua kutumia mtindo wa uzungumzaji ulio tofauti na kundi la watu, jamii au taifa lingine ili kijipambanua na kujitofautisha na wengine.

MAJERELEO

- [1]. BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- [2]. Coates, J. (1986). *Woman, Men and Language Usage: A Sociolinguistic Account of Sex Differences in Language*. New York: Longman Inc.
- [3]. Haas, A. (1979). *Male and Female spoken Language Defferences: Stereotypes and Evidence*. New York: College of New Paltz.
- [4]. Jespersen, O. (1949). *Modern English Language Grammar on Historical Principle*. New York: Macmilan.
- [5]. Juma, B. (2015). Tofauti ya Kijinsia katika Utumizi wa Lugha ya Kiswahili Kwa Vijana. Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar. (Haijachapishwa).
- [6]. Kin’gei, K. na Kobia J. (2007). *Lugha kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng nchini Kenya. (Katika Nordic Journal of African Studies. Juzuu.16, Namb.3, 320-332).*
- [7]. King’ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: TATAKI.
- [8]. Labov, W. (1966). *The Social Stratification of English in New York City*. Washington: D.C.
- [9]. Matinde, R. (2012). *Dafina ya Lugha: Isimuna Nadharia, kwa Sekondari, na Vyuo vya Kati na Nyuo Vikuu. Mwanza: Serengeti Educational Publishers Ltd.*
- [10]. Mohammed, N. (2013). *Matumizi ya Lughatandawazi katika simu za kiganjani. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. MA. Kiswahili.* (Haijachapishwa).
- [11]. Msanjila, P. Khore, M. na Massamba, B. (2009). *Isimujamii: Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam University Press.
- [12]. Tajfel, H., na Turner, J. C., (1980). *An Intergrative theory of intergroup conflict: The social psychology*. University of Bristol: England.
- [13]. TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.